SwahiliWeb

ELECTRONIC DEPOSITORY AND RESOURCE ARCHIVE

www.swahiliweb.net

Archive: Pat Caplan

Document: Interview with Abdu Bwana and Binti Issa

File reference: SW/PC/13010

This document has been downloaded from the SwahiliWeb archive on the understanding that it is copyright under the laws of the United Kingdom and the Berne Convention, and that no further copying, storage or distribution, in any form or by any means, including electronically, is permitted except under the provisions of fair dealing.

Copyright of all materials deposited with SwahiliWeb remains with the copyright holder. Those seeking copyright and associated permissions will be referred to the copyright holder.

**Interview with husband Abdu Bwana and wife Binti Issa (pseudonyms). Kanga village, 1966. transcribed by Joseph Bwaithondi**

*Abdurahman Kibwana was one of my neighbours. At this time he and his wife binti Ibrahim were quite elderly, but he lived on and was re-interviewed and recorded in 1985*

AB: Babu aliyemzaa baba kwao ni Mlima, Babu aliyemzaa mama kwao ni Mlima.

Kwao wakina mama tena ndio hapa Mlima, kwa mama zao ndio hapa. Na kwa kina baba wamezaliwa hapa tena,huku walikuja kuoa, katika matembezi yao na kazi zao walizokuja nazo siku za mwanzo, ndio wakazaliwa kina baba ,wakazaliwa kina mama,baada ya kina mama ndio tumezaliwa siye tena.

Babu huku aliyemzaa baba na babu huku aliyemzaa mama, huku bibi aliyemzaa mama na huku bibi aliyemzaa baba

PC: Na mama yako?

AB: Mama yangu? Mama yangu binti Omari

PC: Kwa baba hapa Kanga

AB: Huyu mama?

PC: Mh!

AB: Nakwambia mama babaye yupo Mgima

PC: Mgima vilevile

AB: Baba, baba yangu mie ,babaye yupo Mgima. Wakaja kuzaliwa baba yangu na mama yangu wakazaliwa huku.

PC: Eeh sawa.

PC: Katika nyinyi mkubwa nani wewe katika ndugu na kaka na dada

AB: Ndugu na kaka yangu

AB: Nina kaka yangu anaitwa bwana Omari bin Abrahamani, mimi binti Abrahamani

PC: Baada ya yeye ndio wewe

AB: Ndio.

PC: Baada ya wewe ndio nani?

AB: Kaja mwenzangu bibi

 ©Pat Caplan 2013

PC: Mh!

AB: Binti  Athumani

PC: Baba mbalimbali

AB: Baba mbalimbali, Sie tu wawili tumezaliwa na Baba mmoja Abrahamani

Na huku walipozaliwa na mama baba yao mbali.

PC: Huyu Bwana Athmani

AB: Mh!

AB: Athmani Nyatanga, Juma Nyatanda

PC: Sasa mama na baba waliachana

AB: Ehe waliachana kwa ugonjwa.

PC:  Ugonjwa?

AB: Aliugua mama, alipokuwa mjamzito wa mimba yangu mie, na baba naye alikua mgonjwa, akitoka akienda Dar es salaam. Baade nikizaliwa mie tena huku. Na aliporudi tu wakaachana. Baadae akaja mwenzangu bin Athmani na kwa bahati mbaya naye wakaachana.

PC: Hivyo!

AB: Naye akaja kuoa tena na  baadae akaja Baba yao Juma Nyantanda

PC: Hivyo! , huyu kina Jumbe marehemu.

AB: Baba mmoja mama mmoja

PC: Mh!

AB: Baba yao mmoja mama yao mmoja. Hao ndio ndugu zngu hao.

PC: Ulipokuwa mtoto mdogo uliishi wapi?

AB: Hapa hapa, mpaka nimekuja kuolewa

PC: Na ulipokuwa mtoto mdogo ulikuwa unafanya nini?

AB: Nilikuwa nacheza  michanga tu.

Kicheko

PC: Halafu


©Pat Caplan 2013

AB: Nilipokuwa mtoto mdogo kabisa nilikuwa nachanganyika na watoto wenzangu na kuchezea michanga yetu miguuni, tunakoka moto, moto kabisa tupike , tupike mchuzi,tupike ugali na tupakue.

Kicheko.

AB: Na tulipokuwa tulipokuwa yanki tena tuliacha kuchezea michanga tulikwenda kutafuta kuni , tulite chakula tutwange na tutengeneze fyagio tufagie.

PC: Hivyo!

AB: Eeh!

AB: Baadae ndio tukaolewa , na maisha yalikuwa tulime, tusuke ukindu/ukili ndio maisha tuliyoendelea nayo mpaka leo hii

PC: Sasa katika ulivyokuwa mkubwa ulichezwa ngoma?

AB: Nilichezwa,

PC: Ulichezewa

AB: Eh! Nilichezwa, nilichezewa

PC: Unakumbuika mpaka leo ilikuwaje?

Kicheko

PC: Unakumbuka?

AB: Nakumbuka, kama nisingekumbuka ningelisema??Kitu ambacho sikumbuku sikijui. Ukifika nyumbani unaambiwa, mambo ya zama na awali, nyimbo za awali ndio walichezwa hawa ndugu zangu, lakini sisi watu watatu, kucha hatuli, unalazwa kitandani, na mkalizaji kitandani anakukakaliza weye. Apikiwe Yule yule alikukalisha wewe,wala hauthubutu hata chakula ndani ya roho hakipiti,una haja huna haja atakwambie yeye mwenyewe aliyekukalisha kama unahaja sema mpaka atakosema ndio kutekeleze

PC: Mh!

AB: Ndio akutoe nje na kikundi chako ukatekeleze haja zako halafu urudi pale pale. Uchezwe ngoma tena ndipo wapiti watu huku watwange watu huku wakasage huku . Na Baadae tena wapange watu huku na huko ukapande mkeka Basi sasa barazani ngoma tena wanaume

Some words are missing

PC: Nguo nyeupe , mweupe, sasa umealikwa, umekaa ndani

AB: Ndani!


©Pat Caplan 2013

AB: Mie baba kafa ameniacha bado mdogo hata sijavunja ungo, sasa msiba amekuja mpaka nikuwe nirudi kwangu mwenyewe au Yule kaka nije naye ndio muozaji Yule ndio nani tena, yupo na wazee.

PC: Katika kualikwa umekaa ndani kama mwezi mmoja auzaidi??

AB: Mwezi mmoja?? Mwaka

PC: Mwaka mzima?

PC: Hivyo

AB: Mwaka wa pili hule ,nimevunja ungo zama za makondeni/ mashamba.

PC: Eeh!

AB: Ndio nikavunja ungo. Sasa nikaja hapa Kanga kuama, kisha kuhama, nikaja hapa kutwisha ngoma. Sasa kutwisha ngoma ya kuhama kabisa kabisa wengine

PC: Na wakati huu ulionaje uliogopa au vipi?

AB: Kuogopa tena kuchezwa ?

PC: Katika kuvunja ungo na kuchezwa ngoma ulikuwa ukiogopa?

AB: Nisiogopeje wakati sijuhi, kwani wakati wa kuchezwa niatafanyaje?

PC: Mh!

AB: Nikaja kuchezeshwa salama mpaka nikarudishwa nyumbani asubuhi yake salama

PC: Halafu ulikaa ndani mwaka mmoja?

AB: Yafika mwaka. Baada tu ya kuisha mavunaji, na nilivyotoka nje tu ndio kuposwa. Na katika maswaiba mengine ndio akafa wifi yangu. Hiyo ndio yapata mwaka mmoja tena. Nilikaa mwaka mmoja.

PC: Na mtu mwenyewe ndio huyu bwana?

AB:Hataa

PC: Nani basi

AB: Babuye baba yule.

PC: Hivyo.

AB: Huyu aliyekuwa hapa akisema ndoa ndoa, ndio nimekuja kuozwa mume wa kwanza.

 ©Pat Caplan 2013

PC: Mmeshiriki nini?

PC: Huyu aliyekuowa ni mtoto mdogo?

AB: Ni mtoto  mdogo ila ni mtoto wa nyumbani

PC: Sasa imekuaje harusi yako?

AB: Harusi??

PC : Unakumbuka siku ya harusi

AB: Nakumbuka

PC: Niambie basi

AB: Harusi kutoka kwa wazee wangu mie, pesa ilikuwa ngoma ya sanda

PC: Mh!

AB: Tukafanya kibarua cha Kulima kupanda

PC: Mh!

AB: Mmh!

PC: Na wakati wa harusi wewe ulikuwa wapi? Ndani?

AB: Niko ndani Mwali   sijatoka  nje toka kuvunja ungo,

PC: Eeh!

AB: Ndio  nitoke tena  nilipokwisha olewa tena.

PC: Eeh!

AB: Kwenda kufanya kazi

PC: Eeh!

PC: Nani alikaa nae? Nani alikaa nawe katika harusi

AB: KAtika harusi?

PC: Eeh!

AB: Eh! Hawapo kamwe, mabibi zangu hawapo wameshakwenda rehemani, Kaburini.

PC: Na walikuja kukuuliza?

AB: Kuniuliza?

PC: Kama unakubali au hawakuja?

AB: Wasijeje?? Waja kuniuliza

PC: Ukasema nini?

AB: Nilisema kwanza hawali mimi sitaki

PC: Hutaki

AB: Sitaki, mie nilishamkataa

PC: Mbona ulisema hutaki?

AB: Sasa sitaki kupata radhi ya wazee.

PC: Lakini ulikuwa hamtaki huyu au hakutaka kuolewa??

AB: Huyu. Sikumtaka mchumba huyu.

PC: Ulimjua/ulimfahamu huyu

AB:Nilimjua nikazaa naye huyu binti yangu

PC: Sasa siku ya harusi imekuaje?Wakakufanyia nini?

AB: Walinifanyia sherehe

PC: Lakini wewe hakuwepo ulikuwa ndani tu

AB: Sherehe wale wanaofanya kuudumia harusi mbali na wanaomuudumia Mwali mbali, na wale wazee wangu walimzaa mama na wazee wangu waliomzaa baba. Sikuwa peke yangu hataa.Shekh kwenye mkeka hatasoma nini?

PC:Mh!

PC: Na siku ile ilikuwa ya kuingia ndani

AB: Ndio ilifanywa hasa.

PC: Uliogopa

AB: Hasa, nisiogope, nakijuaje hicho nitakachokuja kupewa mie, tena nisikiogopeje?

PC: Mmh!

AB: Naogopa hapo, hapo na kulia,utulie cha ajabu bibiyo, mamayo . Wapo wamekuja kwa kazi hiyo hiyo. Ya kuoa, basi. Ikabidi nikubali .Na ikafika siku ya kutoka na siku. Hapo siku moja moja utaweza kukaa na wenzako barazani. Na mie nimeshakuwa mtu mzima na uwanja ni wangu. Nikapambwa,

 ©Pat Caplan 2013

PC: Ukapambwa

AB: Ndio nikapambwa , na miwanja hiyo

PC: Mmh!

AB: Nikasukwasukwa  za kusokota, Nikatia kipini (hereni masikioni) na kutogwa pua

PC: Hii umefanya lini kutoga?

AB: Kutoga  zama zetu sie kutoga! Tulitogwa na kutundikiwa nyasi. Na kwa kujifunza tulichukua karatasi , kuzibutua

PC: Walifanya lini?ulipokuwa mdogo mdogo au ulipokuwa mkubwa?

AB: Wakati tulipokuwa wadogo, na nikipita pita ili name nitizamwe kama nimependeza.

PC: Inauma?

AB: Kwa nini hisiume?. Kwa kawaida kutogwa huwa tunatogwa tukiwa watoto wadogo. ( Hapa anaonyesha maeneo mbali mbali katika mwili wake walipomtoga)

PC: Kakufanyia nani kazi hii ya kutogwa

AB: Wazee wangu(bibi mzaa mama) yeye alikuwa mtogaji.

PC: Lakini hapa kwenye kipini umetogwa? (anaonyesha mahala penyewe)

AB: Kwenye masikio hapa nilitogwa je unapaona

PC: Ndio panaonekana.

AB: Wazee wetu pia walitufunza jinsi ya kutunga shanga na hata alipokuja mume alishanikuta nimeshaweka huu  urembo wa kipini na mikufu. Na zama hizi ziliitwa zama za mikufu ya ndege ndege (za dhahabu)

PC: Za dhahabu.

AB: Hizi dhahabu zilinunuliwa na wazee na pindi muda wetu wa kuolewa ukifika basi huwa tukipewa

PC: Ziko wapi sasa ?(vipini vya dhahabu)

AB: zipo sana, basi mimi nilipata viwili, kimoja nilipo mwangu wakati wa kulewa kwake na kingine hata kilipo sikijuhi. Na yeye alipokiweka na walahatupajuhi pengine alinyan’ganywa au

PC: Je ulikaa katika Fungate


©Pat Caplan 2013

AB: Fungate? Nilikaa siku mbili tatu halafu tukaendelea na shughuli za shamba tena. Maana sikukaa katika kimila.

PC: Na uliposhaolewa na huyu bwana ulimuonaje?

AB: Alikuwa mweusi.

PC: Ndio sababu hakumpenda?

AB: Mmh!

PC: Lakini tabia yake ilikuwaje?

AB: Ilikuwa nzuri, Moyo wake ulikuwa mzuri

PC: Moyo wake ulikuwa mzuri

AB: Ndio.

PC: Sasa mlisikilizana au

AB: Hata sijuhi tena, kataka yeye mwenyewe, si kama mie nilitaka aah! yaani kuna joto tu

PC: Joto gani?

AB: Joto joto tu aibu

PC: Aah!

PC: Sasa ilikuwaje alikuwa anaona wivu , na anakukataza kutoka nje?

AB: Mtu akiniuliza haujambo roho yake ikimuuma na ukiangalia na rangi yangu kama wewe weupe wangu niliotoka nyumbani.Hakupenda nisalimiane na mtu yeyeyote hata ndugu zangu hii kutokana na wivu aliokuwa nao. Halikuwa hata jinsi ya kusuka alikuwa anataja anavyotaka yeye na sio ninavyopenda mimi. Pia sikuishi pekeyangu tulishi na mkewe.

PC: Sasa wewe ulikuwa mdogo au mkubwa?

AB: Katika wawili?

PC: Eh!

AB: Mie nilikuwa mdogo.

PC: ndio mdogo

AB: Wakati ule alishakuwa na mkewe ndio nikaja olewa mie. Na huyu mwingine ni hivyo hivyo alikuwa na mkewe na kaja kuniowa mie.

PC: Sasa mlikaa katika nyumba moja na mke mwenzako?

 ©Pat Caplan 2013

AB: Mbali mbali. Kila mtu alikuwa anaishi mbali mbali.

PC: Na huyu mke mwenzako ulimjua na mlisikilizana au??

AB: Nilisikilizana nae mpaka  huyu bwana aliponiacha

PC: Alikuacha??

AB: Ndio aliniacha na kunirejea.

PC: Sababu gani ya kukuacha?

AB: Ni moyo wake tu na wivu  manake kama akiona mabinamu wanaume basi moyo wake unamuuma, alikaa na kufikiria kwamba natembea na huyu na Yule na kadhalika. Yaani kama mtu moyo wako haujatulia utakuwa na shida kama hizi.

PC: Sasa kakuacha mara moja tu au mara nyingi?

AB: Mara moja

PC: Mara moja tu? Na kisha akakurejea.

AB: Ndio.

PC: Sasa na wewe ulitaka akurejee au ulitaka watoto

AB: Kulingana na mambo yake aliyonifanyia nilikataa. Lakini hawa wazee

PC: Wazee walitaka urudi

AB: Ndio haswa, Sasa kama hautawaogopa wazee utamwogopa nani?.Na wazee wakaweka mpka baraza wenyewe kujadili hili tatizo.

PC: Sasa huyu bwana ulizaa naye?

AB: Nakwambia huyu bwana nilizaa naye watoto wawili mwanamme na mwanamke. Mwanamme ndio alifika ukubwani ndio huyu mwanamke akafuatia.

PC: Je huyu nae(mume mwingine ) ulizaa nae?

AB: Ndio mtoto mmoja Abrahamani na mimba zingine ziliaribika.

PC: Sasa huyu mwanaume uliyezaa naye yuko wapi?

AB: Amepotea/amekufa

PC: Amekufa

PC: Sasa mwisho ilikuwaje amekuacha kabisaa

AB: Kaniacha kabisa na nikaja kuolewa na mtu mwingine.

 ©Pat Caplan 2013

PC: Huyu bwana uliye naye sasa?

AB: Ndio.

PC: Sababu gani ya kukuacha kabisa?

AB: Sababu kabisa anajua mwenyewe. Tuliishi kwa kupendana na kisha mapenzi yakawa hayako tena. Sasa mkichukiana utakaa??

PC: Uwezi

PC: Sasa alipokuacha ukaenda wapi? Ukaenda kwa wazee??

AB: Nikaenda kwa wazee wangu.

PC: Wakasemaje?

AB: Wasemaje

PC: Sijuhi

AB: Mambo alikuwa akiyatenda  wazee wangu wanayajua hata na wazee wake pia wanajua.

PC: Sasa ulikaa sana kabla ya kuolewa na huyu na huyu bwana

AB: Hata sikukaa sana

PC:  Hakukaa sana

AB:Mh!

PC: Sasa tuseme katika harusi hiyo mtu huyu wametengeneza wazee au umechagua mmwenyewe?

AB: Mwenyewe

PC: Mwenyewe

AB: Mpaka nilipoka sana mpaka nikazaa naye Riziki

PC: Lakini huyu bwana alikuwa na mkewe

AB: Alikuwa na mkewe na alishazaa nae, si mmoja tu wawili ambao nilimkuta nae. Na mwanae mwingine nilikuwa nae mie, huyo jirani yangu alikuwa akilelea pia

PC: Na huyu bibi ulikuwa ukisikilizana nae??

AB: Tulikuwa tunapata nae. Mie habari yangu sio ya kupenda ugomvi na kuweka maneno na wenzangu

PC : Mlikuwa nyumba moja?

 ©Pat Caplan 2013

AB: Hapana. Mie kwangu huku na yeye kwake kule. Kila nikienda shughulini nilikuwa nikifikia kwake. Na yeye akifikia kwangu vile vile.

PC: Watoto wako ulilea mwenyewe

AB: Hawa sikuwalea mwenyewe,  huyu kalelewa kwake kwa baba yao.

Male Voice: Mnaandika nini

PC: Harusi ya kwake.

PC: Umelea watoto wengine au wakwako tu?

AB:Nimewahi kulea  watoto. Huyu wakwangu na wale wengine. Ila kwa kuwa mwenzangu amekufa hawa hawanitaki tu.

PC: Hawakutaki??

AB: Hawanitaki wao na familia zao tu na mie hawanitaki. Lakini huyo mmoja Bakari alhamdulillahi angalau ananikumbuka na mmoja hayupo hapa ila salamu zake nazipata kupitia barua na chumvi sukari ananitumia. Ungwana wake ndio tunaupata. Hakuna kiumeni wala kikeni. Lakini ndugu wa hapa wao hawajali kwa chochote, si kwa uzima si kwa ugonjwa na si kwa chochote kile.

PC: Sasa mama ukitazama siku za nyuma na ukitizama hali ya maisha siku hizi mbele vipi.

AB: Ya nyuma mie na ndugu zangu tukilima pamoja mpunga, mtana tukivuna ikisha mpunga ni muhogo na  tunatia mnazi lakini sasa

PC: Kulima huwezi

AB: Kupika sina wa kunisaidia inabidi nipike

PC: Labda bwana

AB: Bwana ana wake wengine wawili na mie watatu tena

PC: Hivyo. Sasa anakutwangia nani?

AB: Sasa ni wale wajukuu zangu watoto wa wanangu ndio wakisaidia wanapokuja kukaa na bibi yao

PC: Ndio wanasaidia saidia.

AB: Ndio, hapa jana alipokuja huku nduguyo Mzee nilimuomba mwanae mmoja haje kunikokea moto. Nitakapokuwa sijitambui. Atanifaa hapa na pia ajifunze  kuna wenzie kama hawa hapa pia.


©Pat Caplan 2013

PC: Nataka kukuuliza hivi, bora kuzaliwa mwanamme au mwanamke?? Maisha bora ni ya nani kati ya mwanamke na mwanmme??

AB: Maisha ya mwanammke au mwanaumme siyajuhi, anayajua mwenyewe Mungu. Nilipozaliwa nilimkuta kaka ndio kanilea mpaka nikaolewa na yeye alitangulia akawaacha wanae ndio mie nimewaoza . Ulimwenguu huu maisha ya mwanadamu ni mwenyewe mwenyezi Mungu anayapanga

PC: Bwana mkubwa je tunaweza kuzungumza kidogo??

BM: Unasemaje?

PC: Nina maswali mawili matatu nataka kukuuliza.

AB: Ana maswali mawili matatu.

BM: Kama yepi maswali yenyewe

AB: Maangazo yote toka wakati wa ujana wako mpaka hivi leo.

PC: Wewe una  nyumba  kipunguni?

BM: Mbili zipo

PC: Wake wawili? Tangu lini?

BM: Tangu nizaliwe

AB: Mmoja kaowa mwaka huu huu

BM: Mmoja 1986 mwaka uliopita na mmoja mwaka 1975

PC: Umezaa nao wote

BM: Hapana ni huyu hapa na Yule niliomuacha

PC: Sababu gani ya kumuacha basi?

BM: Tuliishi kwa muda mrefu mpaka alipofikia hatua ya yeye kuchoka na mie basi tuakaacha

PC: Kwa hiyari yake mwenyewe. Ukaja ukaoa bibi mwingine

BM: Bibi mwingine nimeoa huyu na huyu ninae. Huyu nimeoa mwaka ule mwaka kabla ya vita ya England,

PC: Zamani kweli

BM: Ndio nimemuoa na mwaka uliofuata ikawa vita  na ndio kumzaa Yule mzee. Yule mzee mwaka huo wa vita alikuwa tumboni miezi minne. Nikaapelekwa mpakani. Nikaa miezi miwili nikarudishwa. Nilipokuja tena hapa akazaliwa mzee huyu.

 ©Pat Caplan 2013

PC: Halafu bibi huyu mwingine ukaja kuoa au hakuoa tena?

BM: Miaka kumi iliyopita

PC: Kwa hiyo ulioa wanawake wanne?

BM: Hapana walikuwa watatu. Sasa mimi mwaka ule ............. niliowa bibi akafa

PC: Hakuza nae

BM: Ndio bibi yake mtoto huyu wakike. Yeye hakuzaa na baada ya kufa yeye tena ndio nikaowa bibi huyu mwingine. Mwaka  wa kuamisha

PC: Anaotwaje

BM: binti Maalim

PC: Umezaa nae

BM: Hataa

PC: Mwisho waka jana

BM: Nimeoa mfungo sita

PC: Jina lake nani huyu mama

BM : Binti Khatibu

PC: Huyu bibo,

BM: Hataa, yeye yuko huko huko

PC: Hakuzaa naye

BM: Ndio.

PC: Jumla umeowa wanawake kama watano katika maisha yako

AB: Watano??kama kumi hivi

BM: Wakwanza nimezaa nae watoto watano, wapili nilizaa nae mtoto mmoja, huyu ni bibi wa tatu

NB:

PC = Pat

BM = Abrahaman

AB = Binti Abrahaman


©Pat Caplan 2013